# HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

## MUHTASARI WA KIKAO CHA DHARURA CHA KAMATI YA FEDHA NA UTAWALA KILICHOFANYIKA TAREHE 28.10.2021 KATIKA UKUMBI MKUBWA WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA:-**

1. Mhe. Prof.Davis G. Mwamfupe- Mstahiki Meya - Mwenyekiti
2. Bw. Joseph C. Mafuru - Mkurugenzi wa Jiji - Katibu
3. Mhe. Emmanuel S. Chibago - Naibu Meya - Mjumbe
4. Mhe. Antony P. Mavunde - Mbunge Dodoma Mjini - Mjumbe
5. Mhe. Sospeter N. Mazengo - Mwenyekiti Kamati ya Uchumi, Elimu na Afya - Mjumbe
6. Mhe. Jaffar M. Mwanyemba - Mwenyekiti Kamati ya Mipangomiji na Mazingira - Mjumbe
7. Mhe. Amos A. Mbalanga - Diwani Kata ya K/Ndege - Mjumbe
8. Mhe. CP Gideon M. Nkana - Diwani Kata H/Makulu - Mjumbe
9. Mhe. Shifaa M. Ibrahim - Diwani Kata ya Majengo - Mjumbe
10. Mhe. Awadh Abdallah - Diwani Kata ya Zuzu - Mjumbe
11. Mhe. Beatrice Ngerangera - Diwani Kata ya Miyuji - Mjumbe
12. Mhe. Fatuma Zolo - Diwani Viti Maalum - Mjumbe

**WATAALAM WALIOHUDHURIA:-**

1. Bw. Gerald Ruzika - Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi.
2. Bi. Mary Focus Kimario - Kny: Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi

3. Bw. Michael A. Maganga - Katibu Tawala (Wilaya)
4. Bi. Zaina Kaniki - Kny: Mkuu wa Idara ya Afya na Ustawi wa Jamii
5. Bi. Yustina Munishi - Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika
6. Bi. Asha Same Vuai - Mkuu wa Idara Maendeleo ya Jamii na Vijana
7. Bw. Fredrick Mwakisambwe - Kny: Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari
8. Bw. William Alfayo - Kny: Mkuu wa Idara Mipango Miji, Ardhi na Maliasili
9. Bw. Francis Kaunda - Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji
10. Bw. Dickson Kimaro - Mkuu wa Idara ya Mazingira na Udhibiti wa Taka Ngumu
11. Bi. Selina B. Shirati - Kny: Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi
12. QS. Novatus Iramu - Kny: Mkuu wa Idara ya Ujenzi
13. Bi. Flora S. Sagire - Kny: Mkuu wa Kitengo cha Sheria
14. Bw. Albert Kasoga - Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi
15. Bi. Dorice Nsana - Kny: Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi
16. CPA. Jestina Naftal - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani
17. Bw. Evaristus Desouza - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Nyuki
18. Bw. Joseph Fungo - Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA na Uhusiano
19. Bi. Neema Makinda - Afisa Tawala
20. Bi. Anna Makunja - Afisa Utumishi
21. Bi. Gisela Mmavele - Afisa Malalamiko
22. Bw. Denis Gondwe - Afisa Habari
23. Bi. Sekunda Kasese - Mratibu TASAF

**SEKRETARIETI**

| | |
|---|---|
| 1. Bi. Adelina C. Christian | - Mwandishi wa vikao |
| 2. Bi. Anna M. Masanja | - Mwandishi wa vikao |
| 3. Bw. Samwel J. Mlowa | - Mwandishi wa Vikao |
| 4. Bw. Mello Rasso | - Mwandishi wa vikao |

**MUHT.NA.01/2021/2022/KUFUNGUA KIKAO.**

1.1 Katibu aliwakaribisha wajumbe kwenye kikao cha dharura cha Kamati ya Fedha na Utawala ambacho kilitokana na udharura wa mapokezi ya fedha na Kamati hiyo ndiyo inaomba ridhaa ya kupitisha mipango ya fedha hizo ili zitumike. Pia aliomba ridhaa ya kuongeza agenda ya mapokezi ya fedha Sh. 250,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Afya Chang'ombe Pamoja na ombi la idhini ya kutoa Mkataba wa kupangisha jengo la Halmashauri.

1.2 Baada ya maelezo ya Katibu, alikaribishwa Mstahiki Meya ili afunge kikao. Mstahiki Meya aliwakaribisha Wajumbe na kusema kuwa, tujipange vizuri ili Fedha zilizotumwa zisimamiwe vizuri na kazi ifanyike.

Pia, aliomba ridhaa kwa Wajumbe ya kuongeza agenda mbili alizoomba Katibu. Wajumbe waliridhia.

Baada ya maelezo hayo, Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 4:45 asubuhi.

**MUHT.NA. 02/2021/2022 AGENDA ZILIZOJADILIWA.**

1. Kufungua kikao.
2. Mapokezi ya fedha na maandalizi ya ujenzi wa vyumba vya Madarasa ya kidato cha kwanza na Shule Shikizi kwa mwaka 2022 kwa kutumia fedha za

mpango wa maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO – 19.

3. Taarifa ya mapokezi ya fedha za kampeni ya Chanjo ya UVIKO – 19 kiasi cha Sh. 34,672,970.48
4. Taarifa ya mgawo wa Mbegu za Alizeti zenye Ruzuku ya kiasi cha tani 86 zitakazouzwa kwa bei ya Sh. 3500 kwa kilo.
5. Taarifa ya mapokezi ya fedha Sh. 250,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Afya Chang'ombe.
6. Ombi la idhini ya kutoa Mkataba wa kupangisha jengo la Halmashauri (DODIDECO).
7. Kufunga kikao.

**MUHT.NA.03/2021/2022 MAPOKEZI YA FEDHA NA MAANDALIZI YA UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA YA KIDATO CHA KWANZA NA SHULE SHIKIZI KWA MWAKA 2022 KWA KUTUMIA FEDHA ZA MPANGO WA MAENDELEO KWA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO – 19.**

3.1 Katibu aliwasilisha taarifa tajwa hapo juu na kusema kuwa, Halmashauri ya Jiji la Dodoma ilipokea fedha jumla ya shilingi 2,940,000,000.00 ambapo 2,860,000,000.00 ni kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 143 vya Madarasa pamoja na samani zake kwa Shule za Sekondari na 80,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 4 vya Madarasa kwa shule Shikizi. Fedha hizo zimeingia moja kwa moja kwenye akaunti za Shule. Gharama iliyotolewa kwa ajili ya ujenzi wa chumba kimoja cha Darasa pamoja na samani zake (viti na meza) ni shilingi 20,000,000.00. Katika utekelezaji wa miradi hiyo, Halmashauri imepokea maelekezo kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI Pamoja na PPRA yakiruhusu matumizi ya "*Single Source*".

Alieleza kuwa, Ofisi ya Rais TAMISEMI ilitoa maelekezo yafuatayo: -

i. Kuunda Kamati ya uratibu na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi hiyo.

ii. Kuhakikisha utekelezaji wa miradi unaanza ndani ya wiki mbili mara baada ya fedha kupokelewa.

iii. Kuhakikisha miradi ya ujenzi wa Madarasa inakamilika kabla au ifikapo tarehe 15/12/2021.

iv. Halmashauri inaweza kutumia Wakandarasi wa ndani au utaratibu wa "force account". Msisitizo ni kwamba gharama za utekelezaji kwa kutumia njia yoyote zisizidi makadirio ya fedha zilizotengwa kwa shughuli husika.

v. Utekelezaji wa miradi uzingatie thamani ya fedha na ubora wa miradi.

vi. Mstahiki Meya na Madiwani wote kupitia Kamati zao wahakikishe wanasimamia miradi hiyo kwa kushirikiana na Watendaji wa Halmashauri.

vii. Kuhimiza Wananchi kushiriki ujenzi wa miradi inayoendelea katika maeneo yao na kutoa taarifa endapo kuna ubadhirifu wa fedha.

Katibu alisema kuwa, Baada ya kupata maelekezo hayo, Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji ilianza utekelezaji mara moja ambapo Menejimenti ilifanya kikao na ilipitia Mwongozo wa **PPRA** na Maelekezo kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI katika utekelezaji wa miradi hiyo na kupendekeza mfumo wa "**Single Source**" (Kutumia Wakandarasi) ndiyo utumike.

Menejimenti ilipendekeza kwamba shule hizo zigawanywe katika makundi Matano ambapo Wakandarasi wenye uwezo wapewe kazi hizo kwa kutumia mfumo wa Single Source. Kila Mkandarasi anatarajiwa kupewa zaidi ya madarasa **21** kulingana na uwezo wake. Mapendekezo ya mgawanyo huo ni kama ifuatavyo: -

| Na | SHULE | IDADI YA MADARASA | KIASI KWA DARASA | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | ZUZU | 2 | 20,000,000.00 | 40,000,000.00 |
| 2 | MBALAWALA | 1 | 20,000,000.00 | 20,000,000.00 |
| 3 | NALA | 2 | 20,000,000.00 | 40,000,000.00 |
| 4 | UMONGA | 2 | 20,000,000.00 | 40,000,000.00 |
| 5 | KIZOTA | 7 | 20,000,000.00 | 140,000,000.00 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 6 | CHIGONGWE | 1 | 20,000,000.00 | 20,000,000.00 |
| 7 | LUKUNDO | 8 | 20,000,000.00 | 160,000,000.00 |
| 8 | ITEGA | 4 | 20,000,000.00 | 80,000,000.00 |
| 9 | MNADANI | 4 | 20,000,000.00 | 80,000,000.00 |
| | **JUMLA** | **31** | | **620,000,000.00** |
| 1 | KIKOMBO | 2 | 20,000,000.00 | 40,000,000.00 |
| 2 | BUNGE WASICHANA | 3 | 20,000,000.00 | 60,000,000.00 |
| 3 | IYUMBU | 2 | 20,000,000.00 | 40,000,000.00 |
| 4 | DODOMA | 3 | 20,000,000.00 | 60,000,000.00 |
| 5 | SECHELELA | 4 | 20,000,000.00 | 80,000,000.00 |
| 6 | VIWANDANI | 2 | 20,000,000.00 | 40,000,000.00 |
| 7 | NTYUKA | 1 | 20,000,000.00 | 20,000,000.00 |
| 8 | NGHONGHONA | 4 | 20,000,000.00 | 80,000,000.00 |
| | **JUMLA** | **21** | | **420,000,000.00** |
| 1 | MTUMBA | 1 | 20,000,000.00 | 20,000,000.00 |
| 2 | IPALA | 3 | 20,000,000.00 | 60,000,000.00 |
| 3 | NZUGUNI | 10 | 20,000,000.00 | 200,000,000.00 |
| 4 | MAKOLE | 5 | 20,000,000.00 | 100,000,000.00 |
| 5 | IHUMWA | 4 | 20,000,000.00 | 80,000,000.00 |
| 6 | HOMBOLO | 8 | 20,000,000.00 | 160,000,000.00 |
| 7 | KISASA | 3 | 20,000,000.00 | 60,000,000.00 |
| | JUMLA | 34 | | 680,000,000.00 |
| 1 | MSALATO | 2 | 20,000,000.00 | 40,000,000.00 |
| 2 | CHIKOLE | 3 | 20,000,000.00 | 60,000,000.00 |
| 3 | MIYUJI | 7 | 20,000,000.00 | 140,000,000.00 |
| 4 | MAKUTUPORA | 2 | 20,000,000.00 | 40,000,000.00 |
| 5 | CHIHANGA | 3 | 20,000,000.00 | 60,000,000.00 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 6 | CHINANGALI | 4 | 20,000,000.00 | 80,000,000.00 |
| 7 | MLIMWA | 5 | 20,000,000.00 | 100,000,000.00 |
| 8 | KIWANJA CHA NDEGE | 6 | 20,000,000.00 | 120,000,000.00 |
| | **JUMLA** | **32** | | **640,000,000.00** |
| 1 | MPUNGUZI | 6 | 20,000,000.00 | 120,000,000.00 |
| 2 | WELLA | 2 | 20,000,000.00 | 40,000,000.00 |
| 3 | KIKUYU | 2 | 20,000,000.00 | 40,000,000.00 |
| 4 | HAZINA | 4 | 20,000,000.00 | 80,000,000.00 |
| 5 | MKONZE | 7 | 20,000,000.00 | 140,000,000.00 |
| 6 | MBABALA | 4 | 20,000,000.00 | 80,000,000.00 |
| | **JUMLA** | **25** | | **500,000,000.00** |
| | | | | |
| | **JUMLA KUU** | **143** | | **2,860,000,000.00** |

Kwa upande wa Elimu Msingi kiasi cha shilingi **80,000,000.00** kilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vinne vya Madarasa katika shule shikizi mbili kama ilivyoainishwa katika jedwali hapa chini: -

| NA | JINA LA KITUO SHIKIZI | KATA | SHULE | IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA VITAKAVYOJENGWA | KIASI KWA DARASA | JUMLA YA FEDHA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | NG'UNGUGU | KIKOMBO | KIKOMBO | 2 | 20,000,000.00 | 40,000,000.00 |
| 2 | MKOMBOLA | HOMBOLO BWAWANI | HOMBOLO BWAWANI | 2 | 20,000,000.00 | 40,000,000.00 |
| | **JUMLA** | | | **4** | | **80,000,000.00** |

Tarehe **21/10/2021** kilifanyika kikao kati ya Menejimenti na Wakuu wa Shule kujadili namna ya utekelezaji wa ujenzi wa vyumba vya Madarasa. Kikao hicho pia kiliridhia mapendekezo ya ujenzi huo ufanyike kwa mfumo wa "Single Source".

Katibu alieleza kuwa, katika usimamizi wa miradi huo Timu ya usimamizi ngazi ya Wilaya iliundwa ikijumuisha wafuatao: -

- Mkurugenzi wa Jiji.
- Mchumi wa Jiji.
- Afisa Elimu Sekondari.
- Afisa Elimu Msingi.
- Mhandisi wa Jiji.
- Afisa Ugavi wa Jiji.
- Mthamini Majengo wa Jiji (**QS**).

Pia Wakuu wa Idara watapangiwa Kanda za kusimamia miradi hiyo wakishirikiana na Waheshimiwa Madiwani wa Kata husika pamoja na Viongozi wa Kata na Mitaa.

3.1 Baada ya taarifa kuwasilishwa, Wajumbe walipokea na katika kujadili Wakandarasi walishauri zitolewe barua ya kuwaelekeza kuwa jukumu la ujenzi wa madarasa ni la Kata nzima ikiwemo kamati ya ujenzi. Wajumbe walieleza kuwa kwa upande wa viwandani shughuli iliyopo ni ukarabati wa Madarasa na sio ujenzi. Hivyo, Wajumbe walione hilo kwa kuwa fedha zilizotolewa ni za ujenzi wa Madarasa:

Mtaalam alitoa maelezo kwamba Madarasa yatajengwa Mapya na ukarabati wa Madarasa utaendelea kwa fedha za mapato ya ndani.
Aidha, ilielezwa kuwa watakweda kukagua Shule hiyo ikiwemo na Shule nyingine ambazo zina matatizo kama hayo ili waombe kibali TAMISEMI.

**Umonga Sekondari.**

Ilishauriwa wataalam wafike eneo ilipo Shule hiyo ili waone Madarasa mawili yatakapojengwa eneo lipi kutokana na ufinyu wa eneo.
Akitoa ufafanuzi; Mwenyekiti aliwaagiza wataalamu kufanya tathimini ya hali ilivyo kwenye Shule zote ili kuomba kibali kwa Shule zenye changamoto ya nafasi.

- Wajumbe walishukuru kwa kuweka mfano wa "single souce" Pamoja na kutafuta Wakandarasi wenye uwezo. Aidha, walitaka kujua kama Milioni 20 iliyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Darasa moja kama itatosheleza ujenzi Pamoja na samani zake.

- Wajumbe walipongeza Menejimanti kwa mkakati walioonesha wa ujenzi wa Madarasa. Aidha walitaka kujua wamejipanga vipi kuhusu kuwapa usafiri Wahandisi kwa ajiili ya kusimamia kazi hizo. Ilielezwa kuwa hilo litashughulikiwa ili kuhakikisha kazi zinasimamiwa.
- Aidha, ilishauriwa kuwa, Kwenye kanda tano zilizoandaliwa kwa ajili ya ujenzi wa Madarasa Waheshimiwa Madiwani wawekwe wawili wawili kwa kila kanda kuangalia kazi zinavyotekelezwa.
- Wajumbe walishauri kuwa, iwekwe tahadhari kwa waheshimiwa Madiwani Pamoja na wataalam katika kuwakosoa Wakandarasi katika maeneo ya kazi. Hivyo kazi hiyo ya kushauri Wakandarasi wawaachie wahandisi wenye taaluma hiyo.
- Kuhusu nafasi ya Wananchi kwenye miradi ya ujenzi wa Madarasa, Wajumbe walikubaliana kuwa, ushiriki wao uwe kwenye ulinzi na usalama Pamoja na ufuatiliaji wa miradi. Aidha ilishauriwa Wananchi waelezwe nini kitakachofanyika kwenye Kata zao na fedha zitakazopelekwa. Aidha, ziangaliwe Kata zenye changamoto ya maji ili waongee na DUWASA wafikishe maji ili kuondoa changamoto.
- Kuhusu ushiriki wa Kamati ya Fedha na Utawala kwenye miradi litapangwa na ofisi ya Meya na Mkurugenzi.
- Watendaji wa Kata waliopo maeneo yenye miradi ya ujenzi wa Madarasa wasipangiwe kazi nyingine.
- Kila wiki itolewe taarifa ya ujenzi wa Madarasa, hatua iliyofikiwa kwenye ujenzi na kila Kata Mkandarasi afanye kazi kwa gharama zake.
- Kufikia tarehe 15/12/2021 mwisho wa kukamilisha Madarasa, ila Wajumbe walikubaliana kuwa, wiki mbili kabla kazi iwe imekamilika.

Baada ya majadiliano, Wajumbe walipitisha mapendekezo ya mgawanyo wa fedha za ujenzi wa Madarasa.

**MUHT. NA. 4/2021/2022: TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA KAMPENI YA CHANJO YA UVIKO – 19 KIASI CHA SH. 34,672,970.48**

4.1 Katibu aliwasilisha taarifa tajwa hapo juu na kusema kuwa, Ofisi ya Mganga Mkuu wa Jiji ilipokea fedha kiasi cha Tsh 34,672,970.48 kutoka Wizara ya fedha na Mipango ikiwa ni fedha za uendeshaji wa kampeni ya chanjo ya UVIKO-19 zilizo pokelewa tarehe 28/09/2021 na mchanganuo wa matumizi ni kama ifuatavyo: -

Kwa upande wa timu za usimamizi za Halmashauri (CHMT) fedha hizo zitumike katika shughuli za uhamasishaji kwenye jamii (9,206,181.33), kufanya kikao cha kamati ya afya ya msingi ngazi ya Wilaya (3,830,000.00), usimamizi wa kampeni ya chanjo (2,819,221.32) na usambazaji wa chanjo kabla na wakati wa kampeni (9,217,304.81).

Fedha kiasi cha Sh. 9,600,263,.02 zitawekwa kwenye akaunti za vituo vya kutolea huduma za afya kwa ajili ya malipo ya shuhuli ya kampeni ya Kitaifa ya chanjo ya UVIKO-19 kwa malipo ya Watumishi kwa mgawanyo ufuatao:

i. Asilimia 74 ni malipo ya masaa ya ziada.
ii. Asilimia 26 ni malipo ya nauli.
iii. Risiti ya mapokezi na barua ya maelekezo viliambatanishwa.

4.2 Baada ya taarifa kuwasilishwa, Wajumbe waliipokea, waliipitia na kisha waliipitisha na kusema kuwa, fedha zitumike kama zilivyopangwa.

**MUHT.NA. 05/2021/2022: TAARIFA YA MGAWO WA MBEGU ZA ALIZETI ZENYE RUZUKU YA KIASI CHA TANI 86 ZITAKAZOUZWA KWA BEI YA SH. 3500 KWA KILO.**

5.1 Katibu aliwasilisha taarifa tajwa hapo juu na kusema kuwa.

Mkoa wa Dodoma ni miongoni mwa mikoa ya kimkakati kwa kuongeza uzalishaji wa Alizeti ili kupunguza uhaba wa Mafuta ya Alizeti. Waziri mwenye dhamana ya kilimo alizindua mpango wa usambazaji mbegu za Alizeti katika Mikoa 3, ambayo ni Dodoma, Singida, na Simiyu.

Wizara ya kilimo kupitiia wakala wa mbegu (ASA) walitoa mgawo wa Mbegu za Alizeti kwenye Mkoa ambapo Halmashauri ya Jiji ilipangiwa kupewa kiasi cha tani 86 zitakazouzwa kwa bei ya 3500/= kwa kila Mkulima. Katika uzinduzi huo kiasi cha tani tatu zilitolewa.

Ili kutekeleza azma hiyo kwa ufanisi utaratibu ufuatao utafanyika: -

i. Taarifa zitatolewa kwenye Kata zote za kilimo kuwajulisha wananchi.
ii. Kata zote zitaandikiwa barua kueleza kufanya kikao cha Maendeleo ya Kata cha dharura kwa ajili ya kutekeleza mambo ya haraka likiwepo suala la mbegu za ruzuku.
iii. Wakulima waliosajiliwa kulima Alizeti watapewa kipaumbele kuuziwa kwa bei hiyo ya Sh. 3500 kwa kilo.
iv. Matangazo yatatolewa kwa vipaza sauti kweye Kata.
v. Mbegu hizo zinapatikana Halmashauri Idara ya Kilimo na kwenye Kata ambapo fedha zitakusanywa kwa "POS" mashine.
vi. Baada ya mauzo fedha zitapelekwa Wizara ya Kilimo kwa Wakala wa Mbegu (ASA) kiasi cha Sh. 3200 kwa kilo na 300 zitabaki kama gharama za usambazaji.
vii. Kikao cha Viongozi wa Mkoa, Wilaya na Wataalam kilichofanyika tarehe 23/10/2021 kiliruhusu Mawakala ambao watakubaliana na masharti ya kuuza Tshs. 3500 na kurejesha sh. 300 kwa kila kilo.

5.2 Baada ya taarifa kuwasilishwa, Wajumbe waliipokea, waliipitia na katika kuijadili Wajumbe wakitaka kujua kama mtu ana shamba lipo Kongwa anaruhusiwa kununua mbegu Dodoma au mpaka anunue Kongwa. Ambapo ilielezwa kuwa, utaratibu uliopo ni kuuza mbegu kwa Wakulima waliopo Dodoma na zitauzwa kwa utaratibu wa kutumia mashine za POS ili fedha za Serikali zirudi.

Pia, Wajumbe walitoa tahadhari ya watu wanaoweza kununua Mbegu kwa Sh. 3500/= alafu wakawauzia watu kwa bei Zaidi. Hivyo, kuwe na tahadhari hiyo.

7.2 Baada ya majadiliano, Wajumbe waliagiza kuwa, upangishwaji wa jengo la "DODIDECO" lifuate taratibu za kulipangisha na taarifa ioneshe mambo yafuatayo: -

i. Ukubwa wa eneo.
ii. Kiasi kinacholipwa kwa Mita za Mraba.
iii. Uandishi wa Mkataba uoneshe ukubwa wa eneo na kiasi cha fedha kitakacholipwa.
iv. Muda wa Mkataba.

**MUHT.NA. 8/2021/2022: KUFUNGA KIKAO**

8.1 Kabla ya Katibu kumkaribisha Mwenyekiti ili afunge kikao, aliwaeleza wajumbe kuwa, katika ujenzi wa Madarasa Wananchi waelezwe wajue kitakachofanyika kwenye Kata zao, kuwa na kasi ya ujenzi kwa kiwango kizuri. Baada ya maelezo hayo, Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afunge kikao.

8.2 Mwenyekiti aliwataka Maafisa wote watakao kwenda kusimamia ujenzi wa Madarasa ni lazima waandike kwenye kitabu cha kusaini wageni. Mwisho alifunga kikao saa 6:50 mchana.

**UMETHIBITISHWA NA WAJUMBE NA KUSAINIWA NA:**

**JINA KAMILI:** ...Leonard Rwezaura... **JINA KAMILI:** ...Prof Davis Mwamfupe...

**SAINI:** ...[signature]... **SAINI:** ...[signature]...

**KATIBU** **MWENYEKITI**

**TAREHE** ...15/11/2021...

40